# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

## CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA MKOA WA MANYARA

### MAHITAJI YA MWANAFUNZI WA NGAZI YA KWANZA

1. Unatakiwa kununua vifaa vifuatavyo kwa matumizi yako chuoni.
   i. Mashati mawili meupe ya tetron (mikono mifupi).
   ii. Suruali mbili za dark blue kwa kitambaa cha **ISTEM** namba moja tu,ziwe na rinda mbili, upana chini17" na iwe na pindo chini - pindo la nje (turn up)
   iii. Ovaroli la rangi ya kaki kwa wanafunzi wa Useremala, Ovaroli ya rangi ya dark blue kwa wanafunzi wa fani za uhandisi na Ova Koti la rangi nyeupe kwa fani ya maabara, Ovaroli zote zitumie kitambaa cha **ISTEM** namba moja tu.
   iv. Jozi ya viatu vyeusi vya ngozi vya Kamba na vyenye visigino vifupi (viatu vya usalama vya karakana (safety boot) ni bora zaidi).
   v. Vifaa vya hesabu (Mathematical Set).
   vi. Daftari kubwa 10 (Counter Book).
   vii. Nguo za michezo t/shirt na bukta rangi ya blue na raba nyeusi
   viii. Vifaa vya usafi- Jembe jipya lenye mshikio mrefu, kwanja jipya na fagio la chelewa lenye mshikio wa mti mrefu.
   ix. Mwanafunzi afike na karatasi nyeupe A4 ream moja.
   x. Mwanafunzi wa Bweni anatakiwa kufika na mto wa kulalia, shuka, blanketi, chandarua nyeupe, bakuli, sahani, kikombe na kijiko, ndoo ya kufulia na kuogea, ufagio wa ndani (soft broom) pamoja na brashi gumu la kusugulia sakafu lenye mshikio mrefu (hard broom) pamoja na vifaa vya usafi binafsi
   xi. Mwanafunzi mwenye bima ya afya (NHIF) tayari atawasilisha copy ya kitambulisho na hatalipia chuoni gharama ya bima.
   xii. Mwanafunzi afike na kitambulisho cha taifa (NIDA) au namba ya kitambulisho cha taifa.

2. Gharama nyingine ni kama inavyosomeka kwenye jedwali hapo chini:-

KWA MWANAFUNZI WA BWENI.

| Namba | Mahitaji | Bei | Kiasi | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Sweta | 20,000 | 1 | 20,000 |
| 2 | Nembo | 2,500 | 2 | 5,000 |
| 3 | Ada ya Mafunzo | 60,000 | 1 | 60,000 |
| 4 | Ada ya Bweni | 60,000 | 1 | 60,000 |
| 5 | Kitambulisho | 5,000 | 1 | 5,000 |
| 6 | Fulana | 18,000 | 1 | 18,000 |
| 7 | Bima ya Afya(NHIF) **(NI LAZIMA)** | 50,400 | 1 | 50,400 |
| 8 | Fedha ya Tahadhari | 10,000 | 1 | 10,000 |
| 9 | Michezo | 10,000 | 1 | 10,000 |
| 10 | Godoro | 20,000 | 1 | 20,000 |
| **JUMLA** | | | | **258,400/-** |

Mwanafunzi wa Bweni anatakiwa kulipia jumla ya **Tshs. 258,400/-** kwa mkupuo na hatapokelewa ikiwa hajatimiza kiasi hicho cha fedha na nafasi yake kupewa muombaji mwingine.

KWA WANAFUNZI WA KUTWA

| Namba | Mahitaji | Bei | Kiasi | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Sweta | 20,000 | 1 | 20,000 |
| 2 | Nembo | 2,500 | 2 | 5,000 |
| 3 | Ada ya Mafunzo | 60,000 | 1 | 60,000 |
| 4 | Kitambulisho | 5,000 | 1 | 5,000 |
| 5 | Fulana | 18,000 | 1 | 18,000 |
| 6 | Bima ya Afya(NHIF) **(NI LAZIMA)** | 50,400 | 1 | 50,400 |
| 7 | Fedha ya Tahadhari | 10,000 | 1 | 10,000 |
| 8 | Michezo | 10,000 | 1 | 10,000 |
| **JUMLA** | | | | **178,400/-** |

Mwanafunzi wa kutwa anatakiwa kulipia jumla ya **Tshs. 178,400/-** kwa mkupuo na hatapokelewa ikiwa hajatimiza kiasi hicho cha fedha na nafasi yake kupewa muombaji mwingine.

## GHARAMA NYINGINE

Ada ya mtihani wa taifa wa VETA (CBA) ya Tsh. Elfu ishirini na tano (25,000/-) kwa ngazi ya kwanza italipiwa muhula wa pili wa mafunzo.

## MUHIMU

i. Fedha zote zitalipwa kwenye **"Control No"** atakayopewa mwanafunzi baada ya kuripoti chuoni.
ii. Bima ya afya italipwa kwa Control namba itakayotolewa na NHIF kwa uratibu wa ofisi ya Msajili chuoni

## CHUO CHA UFUNDI STADI NA HUDUMA MKOA WA MANYARA

### SHERIA ZA CHUO:

Ili kufanikisha mafunzo ya ufundi stadi kila mwanafunzi anatakiwa kufuata sheria zifuatazo:-

1. **MAHUDHURIO:**

(a) Kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1:30 asubuhi. Hii ina maana ifikapo saa 1:30 asubuhi wanafunzi wote wawe wameshafika chuoni. **ADHABU KALI ITATOLEWA KWA WACHELEWAJI**.

(b) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani, hospitali Au sehemu nyingine yoyote ile bila ya kuruhusiwa na Mwalimu wa zamu kupitia kwa mwalimu wa darasa.

(c) **Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuugua mwenyewe ni lazima habari/taarifa zifike chuoni, bila ya kufanya hivyo ni kosa.**

(d) Mahudhurio chini ya 85% mwanafunzi atanyimwa cheti cha kuhitimu mafunzo.

2. **MAVAZI:**

(a) Sare ya chuo ni suruali ya dark bluu na shati jeupe la mikono mifupi na T-shirt ya VETA. Sare hiyo ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo chuoni na wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani. Wakati wote shati liwe limechomekewa.

(b) Ovaroli livaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu.

(c) Viatu vyenye visigino virefu na kanda mbili au viatu vya wazi (sandals) haviruhusiwi kuvaliwa chuoni.

(d) Vifaa vya usalama vivaliwe kikamilifu wakati wote wa mafunzo kwenye karakana.

3. **USAFI WA MWILI:**

(a) Hairuhusiwi kuvaa hereni, pete, bangili na mapambo ya aina yoyote ile kwa kipindi chote cha mafunzo.
Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanayotoa harufu kali.

(b) **NYWELE KWA WAVULANA:**

i. Zikatwe ziwe fupi sana, KIPARA hairuhusiwi kabisa.
ii. Ndevu haziruhusiwi. Ndevu za aina zote haziruhusiwi mustachi/sharubu.

(c) **NYWELE KWA WASICHANA:**

i. Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari ya kurudi nyuma.
ii. kucha zisifugwe kabisa wala kupaka rangi

4. **WIZI WA MALI ZA CHUO AU MALI YA MTU YEYOTE YULE:**

(a) Vitendo vyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika mwanafunzi ameiba mali ya chuo au mwanafunzi mwenzake, basi atafukuzwa chuo mara moja na kufikishwa kwenye vyombo vya dola.

(b) Ukipoteza kifaa cha chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa na ukakinunue kifaa chenyewe au ulete badala ya ulichokipoteza.

(c) Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo.

(d) Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na getini.

5. **UGOMVI:**

Ugomvi, kupigana au kushambuliana ni makosa ya jinai. Atakayepatikana akijihusisha na matendo ya namna hiyo atafukuzwa chuoni na kukabidhiwa kwenye vyombo vya dola.

6. **ULEVI:**

Iwapo itabainika mwanafunzi analewa au kuonekana katika sehemu za vileo, anavuta bangi au madawa ya kulevya adhabu yake ni kufukuzwa chuo mara moja.

7. **MAPENZI:**

(a) Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi/mwalimu na mwanafunzi hairuhusiwi kabisa.

(b) Mwanafunzi wa kiume au wa kike haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi watumishi bila ya kibali au ruhusa.

8. **MIGOMO:**

Migomo ni marufuku, na kuchochea migomo ni kosa lisilostahimilika. Atakayeshawishi au kusababisha migomo atafukuzwa chuoni mara moja.

9. **LUGHA:**

Lugha inayotumika kuendeshea masomo ni kiingereza hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kujifunza kiingereza.

10. **KUBADILI JINA**

Jina lisibadilishwe mpaka ziwepo sababu na hati maalum kwa uthibitisho na ajulishwe Mkuu wa Chuo mara moja.

11. **MATUMIZI YA SIMU DARASANI**

I. Ni marufuku kuwasha simu za mkononi wakati wote wa vipindi.
II. Ni marufuku kuweka visikilizia sauti masikioni (Earpods na Earphones) wakati wote wa vipindi chuoni.

12. **USAFI WA MAZINGIRA**

I. Usafi wa maeneo yote ya chuo ni wajibu wa kila mwanafunzi hivyo unawajibika kila wakati kutunza bustani, kufagia na kufyeka nyasi maeneo yote ya ndani ya chuo na eneo linalozunguka chuo
II. Ni marufuku kushika au kukanyaga kuta za majengo maeneo ya karakana na ofisi
III. Husuhusiwi kukatisha maeneo ya bustani au sehemu zilizopandwa nyasi, unatakiwa kutumia njia husika tu.
IV. Ni marufuku kuingia darasani au karakana na aina yeyote ya kimiminika, chakula, bazooka n.k
V. Unatakiwa kutupa takataka sehemu huzika za kutupa taka na si vinginevyo.

**ONGEZEKO LA SHERIA KWA WANACHUO WA BWENI**

13. Mwanachuo ataruhusiwa kutoka nje ya Chuo siku zifuatazo tu:

    i. Jumapili na siku za sikukuu za kitaifa kuanzia saa 12.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni
    ii. Jumamosi kuanzia saa 7:30 mchana hadi saa 12 jioni
    iii. Hairuhusiwi kutoka nje ya Chuo wakati wowote bila kibali maalum.

14. Mwanachuo yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya eneo la Chuo anapaswa kuwa na kitambulisho cha Chuo na atajiandikisha lango kuu na sare ya Chuo. Mwanafunzi atakayeonekana nje ya maeneo ya Chuo bila kitambulisho atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa nafasi ya kulala bwenini au kufukuzwa chuoni.

15. Mwanachuo atakayepatikana na kosa la kulala au kuwa nje ya Chuo bila kibali atasimamishwa masomo.

16. Hairuhusiwi kupikia chakula bwenini, na atakayekiuka sheria hii atachukuliwa hatua kali.

17 (a) Ni marufuku wanachuo wa kiume na wakike kutembeleana mabwenini.

   (b) Hairuhusiwi **KABISA** kwa mwanachuo kuingia katika eneo wanamoishi wafanyakazi wa Chuo bila ruhusa au kibali.

18 Hairuhusiwi kupeleka chakula bwenini. Endapo kuna mgonjwa, ruhusa maalum kutoka kwa Mwalimu wa zamu/Mlezi wa wanafunzi itatolewa.

19 Taa za madarasani na mabwenini zizimwe saa 4:00 za usiku.

20. Hakuna ruhusa kumkaribisha au kumlaza mgeni, ikiwa mwanachuo atatembelewa na mgeni au ndugu siku ya masomo, ni lazima kumjulisha mwalimu wa zamu kabla ya kumkaribisha katika sehemu ya mazungumzo.

    - Wageni wanaruhusiwa kuwatembelea ndugu zao kila Jumamosi kuanzia saa 7:00 mchana hadi saa 12:00 jioni.
    - Kila Jumapili na siku za sikukuu kuanzia saa 12:00 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni.

21. Vyumba/Madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya Chuo.

22. Ruhusa ya kulala nje ya mipaka ya Chuo itatolewa na Ofisi ya Mkuu wa Chuo.

..............................................

Principal
VETA Manyara RVTSC
P.O. Box 485
BABATI

**NANSANGA GODWIN MASSANGYA**

**K/MKUU WA CHUO**

VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY

MEDICAL EXAMINATION FORM

**Date...................................**

THE MEDICAL OFFICER

..................................................................

.................................................................

................................................................

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION:**

Name of trainee ..................................................................

Please examine the above named trainee to his/her fitness to undergo training and subsequently work as a/an.............................................................................

Eyesight...........................................................

Hearing.............................................................

Asthma..............................................................

Other serious diseases.......................................

MEDICAL CERTIFICATE:

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for training as above.

Date .......................................... Designation..................................................

Signature and official stamp.................................................

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

**a) MWANACHUO**

Mimi ..................................................Fani ya ..................................................ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa, pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za chuo ambazo nimezisoma na kuzielewa vizuri.

Sahihi ..........................................   Tarehe ..............................

**b) MDHAMINI**

Mimi ...........................................................................................................................
ambaye(Mzazi/Mlezi/Kaka/Dada n.k) ...........................................................wa mtajwa hapo juu nathibitisha kuwa ninamdhamini na nitamlipia gharama zote za mafunzo ikiwa ada na michango mingine kama ilivyoelekezwa katika maelezo ya kujiunga na Chuo wakati wote wa mafunzo.

Simu........................................................

Sahihi ..........................................   Tarehe ..............................